



TAMONGSCO

Tanzania association of managers and owners of non-government schools and colleges

For equitable access to quality education

I J U E **TAMONGSCO** NA ELIMU BORA KWA WOTE

Kanda ya «ZoneKiswahili»

P.O.Box 63088, Dar Es salaam
E.mail: sg@tamongsco.org

1. SEKTA BINAFSI NA ELIMU

Watoaji wa elimu katika sekta isiyogharamiwa na serikali wameweza kuwa na manufaa yafuatayo katika Taifa letu la Tanzania ambayo yasingepatikana bila sekta hii kuwepo: -

- 1.1. Imeongeza pato la Taifa kwani wafanyakazi ambao wameajiriwa katika sekta hulipa kodi kutokana na mishahara. Aidha, imeongeza fedha za kigeni kwani kuna wanafunzi wanaotoka nchi za jirani ambao wanakuja kutafuta elimu bora hapa katika shule za TAMONGSCO.
- 1.2. Imepunguza matumizi ya fedha ya kigeni kwani wanafunzi waliokuwa wanaliipiwa nje ya nchi kwa ajili ya kupata elimu bora sasa wanaipata elimu hiyo hapa hapa nchini.
- 1.3. Imepunguza vibaka kwani wanfunzi ambao hawakupata nafasi kusoma katika shule za serikali wamepata nafasi hizo katika shule/vyuo visivyo nya serikali
- 1.4. Imehifadhi mila na desturi za kitanzania kwani wanafunzi waliokuwa wakiharibiwa mila kwa kwenda nje ya nchi kutafuta elimu bora sasa wanapata elimu bora hapa hapa Tanzania
- 1.5. Sekta hii inatoa ajira kwa wazawa
- 1.6. Inapunguza unyonywaji wa rasilimali watu (brain drain) ambao, kama shule/vyuo hivi visingekuwepo wangekwenda nje ya nchi kutafuta mishahara mizuri.

2. TAMONGSCO NI NINI?

TAMONGSCO ni shirikisho la wamiliki na mameneja wa shule na vyuo visivyo nya serikali. Shirikisho hili lilianzishwa hapa Tanzania mwaka 1998 na kusajiliwa mwaka 2001 wizara ya mambo ya ndani kama asasi isiyo ya kiserikali (NGO). TAMONGSCO ina katiba yake na kanuni mbalimbali za uendeshaji. Kwa mujibu wa katiba hiyo,

shirikisho hili hufanya mikutano yake katika ngazi za wilaya, mikoa, kanda na Taifa.

Wanachama wa TAMONGSCO ni asasi zote zinazomiliki taasisi zitoazo elimu katika ngazi za shule (msingi na sekondari), vyuo nya kawaida na vyuo vikuu. Hadi sasa TAMONGSCO ina wanachama zaidi ya 2,000 ambao ni mashirika ya dini (makanisa, misikit na asasi zingine za dini), asasi zisizo za serikali (NGO¹, FBO², trusts), Jumuiya ya wazazi (TAPA³), jeshi la wananchi wa Tanzania (JWTZ/TPDF⁴), magereza, makampuni na watu binafsi.

Kutokana na kasi kubwa ya kuongezeka kwa wanachama wake katika kila wilaya nchini kote, TAMONGSCO imeongeza kanda zake kutoka nane hadi kumi na moja ambapo kila kanda ina mkoa mmoja hadi mitatu. Pia tunashirikiana na jumuiya ya mashule binafsi ya Zanzibar (ZAPS⁵).

TAMONGSCO pia hufanya kazi kupitia sekta ndogo za elimu ambazo pia zina vyama vyake kwa ngazi ya shule za msingi (NGOPSO⁶), sekondari (OHONGSS⁷) na vyuo (ONGCOM⁸)

3. MALENGO YA TAMONGSCO

TAMONGSCO ilianzishwa kwa njozi ya kuona wasichana na wavulana wa kitanzania wakipata elimu bora kwa usawia. Ili kufikia njozi hii, TAMONGSCO imojiwekea malengo yafuatayo: -

- 3.1 Kuweka mahuiano ya kudumu katika serikali na wamiliki wa shule/vyuo kwa njia

¹ NGO = Non-government organization

² FBO = Faith Based Organization

³ TAPA = Tanzania Parents Association

⁴ TPDF = Tanzania People's Defence Forces

⁵ ZAPS = Zanzibar Association of Private Schools

⁶ NGOPSO = Non-government primary schools organization

⁷ OHONGSS = Organization of heads of non-government secondary schools

⁸ ONGCOM = Organization for non-government college owners and managers

ya miundo ya majadiliano ya kisera (policy dialogue structures)

3.2 Kutoa taarifa kwa wanachama kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu utoaji wa elimu.

3.3 Kushirikiana na asasi mbalimbali ndani na nje ya nchi

3.4 Kutoa machapisho mbalimbali yahusuyo elimu

3.5 Kuanzisha kituo cha utoaji wa taarifa za kuwezesha waalimu kufanya vizuri zaidi katika ufundishaji

3.6 Kushirikiana na serikali katika kuboresha sera za utoaji wa elimu

3.7 Kushirikiana na wakuu wa shule/vyuo katika usimamizi wa elimu

4. UNAKUWAJE MWANACHAMA?

4.1 Kutambuliwa na serikali kama mmiliki au meneja wa shule au chuo.

4.2 Kulipa kiingilio cha Tshs 100,000/= (Mara moja tu) na ada ya kila mwaka ya Tshs 300,000/= kupitia akaunti ya CRDB 01J1005130900 iitwayo "TAMONGSCO". Kwenye hati ya Benki, hakikisha umeandika jina la asasi inayomiliki shule/chuo kwa ada ya uanachama na jina la shule kama ni ada ya kila mwaka.

5. NINI KAZI ZA TAMONGSCO

Kama zilivyo asasi zingine zisizo za serikali, TAMONGSCO ni chombo kinachoshughulikia maslahi na maendeleo ya wanachama wake; ikiwa ni pamoja na kero zinazowakibili. Baadhi ya kero ambazo TAMONGSCO inazishughulikia kwa niaba ya wanachama wake kwa sasa ni kama ifuatavyo: -

7.1. Mashule/vyuo visivyo vya serikali kukosa ruzuku ya za uendeshaji wa shule

7.2. Riba kubwa zitolewazo na mabenki kwa shule/vyuo visivyo vya serikali

7.3. Mashule/vyuo kulazimishwa kulipa kodi ambazo zimesamehewa kisheria

7.4. Ugumu na gharama kubwa ya upatikanaji wa vibali vyaa waalimu wasio watanzania

7.5. Mabadiliko ya mitaala ya mara kwa mara yanayofanywa na serikali bila kushirikisha wadau

7.6. Utungaji mbovu wa mitihani ya Taifa inayofanya mwanafunzi afaulu katika ngazi moja na kushindwa kuendelea katika ngazi inayofuata.

6. UNANUEAIKAJE?

TAMONGSCO ndio msemaji pekee wa wamiliki na mameneja wa shule/vyuo binafsi katika majadiliano na serikali pamoja na mashirika mengine yenye malengo yanayofanana na ya TAMONGSCO. Hivyo kwa kuijunga na TAMONGSCO, utanufaika na yafuatayo: -

6.1 Kupata fursa ya kufanya ziara katika nchi jirani kujifunza kwa wenzetu namna wanavyoendesha shule/vyuo vyao. TAMONGSCO ina ushrikiano na asasi mbalimbali ndani ya nchi (TEN/MET¹), nchi jirani kama Kenya (KAEAM²), Malawi (ISAMA³), Zambia (ISAZA⁴) Afrika ya kusini (ISASA⁵), jumuiya ya maendeleo ya nchi za kusini mwa Afrika (SADC⁶), shirikisho la watoaji wa elimu wasiofadhiliwa na serikali kusini mwa jangwa la Sahara (CIEPSSA⁷) na

¹ TEN/MET = Tanzania education network/mtandao wa elimu Tanzania

² KAEAM = Kenya association for education administration and management

³ ISAMA = Independent schools association of Malawi

⁴ ISAZA = Independent schools association of Zambia

⁵ ISASA = Independent schools association of Southern Africa

⁶ SADC = Southern Africa development community

⁷ CIEPSSA = Consortium for independent education providers in Sub-Saharan Africa

shirikisho la wasimamizi na watawala katika elimu katika jumuiya ya madola (CCEAM⁸)

6.2 Kushirikisha shule yako katika mitihani ya ujirani mwema na mashindano mengine kama mpira, mijadala ya hoja n.k.

6.3 Mawazo na kero zako kupelekwa kwenye mamlaka husika.

6.4 Kuhudhuria mikutano mbalimbali na kubadilishana mawazo na wamiliki wengine

6.5 Kupata nafasi ya kupiga kura au kuchaguliwa kuwa kiongozi katika ngazi mbalimbali

7. NANI KIONGOZI WAKO?

7.1. Ngazi ya Taifa

Katika mkutano wake uliofanyika Julai 27-29, 2011 pale Triple "A" club, Sakina, Arusha, viongozi wafuataao walichaguliwa

- | | |
|---------------|-------------------|
| i. Mwenyekiti | Alfred G. Luvanda |
| ii. Makamu | |
| iii. Katibu | |
| iv. Naibu | Sigreti Ntungi |
| v. Mhazini | |
| vi. Msaidizi | |

7.2. Ngazi ya kanda ya «ZoneKiswahili»

Ukiondoa mwenyekiti ambaye alichaguliwa katika mkutano mkuu wa Taifa, viongozi wafuataao walichaguliwa katika mikutano ya kanda.

- | | |
|-------------|-------|
| i. M/kiti | |
| ii. Makamu | |
| iii. Katibu | |
| iv. Makamu | |
| v. Mhazini | |
| vi. Makamu | |



⁸ CCEAM = Commonwealth consortium for education administration and management